HOTUBA YA UFUNGUZI WA WARSHA YA MAJADILIANO YA WADAU KUHUSU MCHAKATO WA AJENDA YA MAENDELEO BAADA YA MALENGO YA MILENIA 2015

MGENI RASMI (MKUU WA MKOA)

Veta Conference Hall, Mtwara

4 Disemba, 2012

Ndugu wageni, wawakilishi wa serikali za mitaa katika ngazi za mikoa, wilaya, kata na vijiji, wawakilishi wa asasi za kiraia pamoja na walengwa wao, waandishi wa habari kutoka katika ngazi zote, mabibi na mabwana. Protokali imezingatiwa.

Malengo ya Milenia ni matokeo ya Mkutano wa Kilele wa Milenia wa Umoja wa Mataifa uliofanyika mwezi wa tisa mwaka 2000, uliowakutanisha pamoja wakuu wa nchi 147, waliokuwa wakiwakilisha Mataifa Wanachama 189 wa Umoja wa Mataifa. Lengo kuu lilikuwa ni kufafanua mkakati wa pamoja wa vipaumbele juu ya jinsi ya kuondoa umaskini duniani na kuleta maendeleo katika jamii.

Mpango wa Malengo ya milenia unatoa wito kwa nchi zinazoendelea na zilizoendelea kufanya kazi kwa kushirikiana ili kufikia malengo ya kupunguza umaskini, njaa, magonjwa, pia kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano , kuhakikisha elimu ya msingi kwa watoto, fursa sawa kwa wanawake, na mazingira bora ya kuunga mkono maendeleo endelevu.

Tanzania ni kati ya nchi zilizoitikia wito wa Malengo ya Milenia, na imefanya vizuri katika maeneo mengi, ingawaje matokeo katika baadhi ya maeneo sio ya kuridhisha. Kwa mfano:

- Umasikini wa Huduma Muhimu (Basic Needs Poverty) umepungua toka asilimia 39 katika mwaka 1990 kwenda asilimia 33.6 katika mwaka 2007. Lengo kwa Tanzania lilikuwa kufikia asilimia 19.5 ifikapo mwaka 2015.
- Uandikishwaji wa watoto katika shule za msingi umeongezeka toka asilimia 54.2 katika mwaka 1990 kwenda asilimia 95.4 katika mwaka 2010. Lengo lilikuwa kufikia asilimia 100 katika mwaka 2015.
- Vifo vya watoto wachanga vimepungua kutoka watoto 115 katika 1000 (mwaka 1990) hadi watoto 51 katika watoto 1000 (mwaka 2010). Lengo lilikuwa kufikia vifo 38 katika watoto 1000 ifikapo mwaka 2015.

Haya ni baadhi ya mafanikio yaliyoonekana hapa nchini. Hata hivyo umasikini hapa Tanzania umepungua kwa kiasi kidogo sana ukilinganisha na kukua kwa pato la Taifa. Pato la taifa limeongezeka kutoka asilimia 1.6 mwaka 1992 hadi kufikia asilimia 7.0 mwaka 2010, lakini umasikini umepungua kwa kiasi cha asilimia 2.9 tu katika kipindi hichohicho. Na hili ndilo tatizo kubwa linaloonekana kuendelea kuathiri maendeleo na ustawi wa jamii yetu hapa Tanzania.

Utekelezaji wa Malengo ya Milenia Tanzania umekuwa ukifanyika kupitia utekelezaji wa sera na mikakati ya kitaifa. Kwa mfano, utekelezaji wa Dira ya

Taifa – 2025 na Dira ya Zanzibar – 2020 ni utekelezaji wa Malengo ya Milenia kwa kiasi fulani. Vilevile, utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania (MKUKUTA I na II), pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Muda mrefu (2010 – 2025) pamoja na Mipango ya maendeleo ya muda wa kati (2010-2015; 2015-2020; na 2020-2025), ni sehemu kubwa ya utekelezaji wa Malengo ya Milenia.

Kwa kuwa sasa hivi tunakaribia kufikia mwaka wa Malengo ya Milenia – mwaka 2015 (maana bado takribani miaka 3), na kwa kuwa baadhi ya nchi bado hazielekei kuyafikia Malengo ya Milenia ifikapo 2015 kama tunavyotegemea, watu na taasisi mbalimbali duniani wameshaanza kujadili na kujiuliza – kitatokea nini baada ya mwaka 2015! Wengine wameulizia nini kifanyike baada ya mwaka 2015 ili kuongeza kasi na kutoa msukumo wa maendeleo duniani nk.

Maswali hayo yamepelekea serikali yetu kuagiza kuwa wadau mbalimbali katika nchi yetu washirikishwe katika majadiliano hayo ili waweze kutoa vipaumbele vya kitaifa na kupanga mikakati endelevu ambayo wadau wenyewe wanaamini kuwa itakuwa na ufanisi. Taarifa itakayotokana na majadiliano haya, itakuwa mchango wa Tanzania katika kuandaa mikakati mipya na malengo mapya tunayoamini yatatoa msukumo wa kimaendeleo duniani kote, hususani katika nchi husika.

Katika kutekeleza hilo, Taasisi ya Utafiti wa Mambo ya Uchumi na Jamii (Economic and Social Research Foundation – ESRF) imepewa jukumu na Ofisi ya Raisi, Tume ya Mipango kukusanya maoni ya wadau mbalimbali kupitia

warsha kutoka katika mikoa yote ya Tanzania. Warsha hizi zinakutanisha wadau na maafisa wa serikali za mitaa na asasi za kiraia na wananchi. Hivyo basi, ushauri na mapendekezo yenu ya nini kifanyike kwa siku zijazo baada ya 2015 ni muhimu sana. Ni muhimu muongozo wa hoja na mapendekezo yaongozwe na maswali yafuatayo:

- Ni vitu gani vinasababisha umasikini kuzidi kuathiri jamii zetu?
- Mambo gani yanatakiwa yafanyike ili kukiwezesha kizazi kijacho kuishi vizuri hapa nchini au katika jamii tunazotoka?
- Ni mambo yapi katika jamii tunazotoka ni muhimu kuyahifadhi (au kuyaendeleza) ili kuwawezesha watu kuishi maisha mazuri na bora?
- Tunafikiri ni watu gani watatakiwa au taasisi zipi zitapaswa kufanya maisha bora kwa jamii zetu yapatikane, na wanahitaji kufanya nini?
- Tutahakikishaje kuwa tumefanikisha au hatujafanikisha azma zetu hizi za maisha bora katika jamii?
- Na mwisho, twafikiri taasisi hizo zinahitaji msaada gani ili kuweza kufanikisha majukumu hayo?

Kwa maneno haya machache nachukua fursa hii kuwakaribisha rasmi katika mjadala huu na kuwaomba mshiriki kikamilifu ili tuweze kupata kile tunachokihitaji katika kuleta maendeleo nchini mwetu.

Baada ya kusema hayo, ndugu waalikwa, mabibi na mabwana ningependa kutamka kuwa warsha hii imefunguliwa rasmi. Nawatakieni majadiliano yenye mafanikio.

Asanteni sana.